

NI MIMI

 Ningetaka, kama mkitaka kufungua pamoja nami katika Mathayo mlango wa 14. Tunataka kusoma sehemu tu hapa, kwa ajili ya mpangilio mdogo, wa mazungumzo ya dakika chache tu kabla hatujaitisha mstari wa maombi. Basi mwanangu alisambaza kadi za maombi muda mfupi uliopita kwa watu ili tuweze kufanyiza mstari, na kuwaombea katika muda mfupi. Tufungue sasa Mathayo mlango wa 14, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 22:

Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni, na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano.

Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda... m—mlimani faraghani, kwenda kuomba: na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.

Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi: maana upepo ulikuwa wa mbisho.

Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaenda, akienda kwa miguu juu ya bahari.

Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.

Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msioCOPE.

2 Na kama nikiliita somo, ningetaka kuchukua somo: *Ni Mimi.*

3 Hapana shaka ilikuwa karibu wakati jua lilipokuwa likitua wakati ule mgongo mkubwa, mgumu, uliojaa misuli wa yule mvuvi mkubwa ulipoanza kusukuma kifundo cha maskini mtumbwi huo majini. Na kama vile ninavyoweza kumwona, wakati akiuelekeza baharini, aliupanda mwenyewe, na yapata katikati ya huo mtumbwi akachukua kiti chake karibu na Andrea, ndugu yake, akaketi. Nao ulikuwa wa kuendeshwa na mwanadamu, nao wakaanza kutumbukiza makasia yao majini, huku ukifanya mawimbi yake madogo ukivuka bahari.

4 Na, bila shaka, umati uliosimama ukingoni ulikuwa tu, walishangazwa, walistaajabishwa alasiri hiyo, walipokuwa wakiona ishara kuu na maajabu kwa watu hawa. Wengi wa Israeli walikuwa wakishangilia siku hizo. Na walipokuwa wamesimama ukingoni, maelfu ya watu wakipunga mikono yao na kuwaaga, na, “Harakisheni mrudi,” kama vile watu wengi wangepanya baada ya kundi la wahudumu kuwako, na kufanya,

na kutenda miongoni mwa watu, kama walivyoona yakitendeka siku hiyo.

⁵ Ninaweza kuwazia mara moja moja, kumwona mtu mmoja akiachilia kasia lake, na kuwapungia mkono pia, kisha mtu fulani ukingoni akipunga mkono, na, kupeperusha lesa zao, na kadhalika, wakati hiyo meli ndogo ilipoanza kuvuka bahari.

⁶ Baada ya kitambo kidogo, labda, walikuwa hawaonekani kabisa kutoka ufukoni, huku makutano wakianza kuelekea makwao, hebu tuwazie ilikuwa ni kimya cha muda mrefu sana, hakuna mtu aliyesema lolote, utusitusi wa jioni ukaingia, hapana shaka ilikuwa ni yule kijana Yohana, akiwa ndiye mdogo zaidi wa kundi hilo, aliyeacha kupiga makasia, na kupangusa jasho usoni mwake, na kusema, “Enyi watoto wa Ibrahimu, na ndugu zangu, tunaweza kuwa na hakika sasa ya kwamba hatufuati namna fulani ya mlokole, ya kwamba Mtu huyu ni kile tu Yeye asemacho ndicho alichu. Yeye si mlokole, kama wengi wa watu wetu wanavyoamini siku hizi, wala Yeye si nabii wa uongo.

⁷ “Ninaweza kukumbuka,” angesema, “nilipokuwa tu mvulana mdogo, wakati mama yangu mrembo wa Kiebrania alipokuwa akiniweka pajani mwake, na kunisimulia hadithi za Agano la Kale, jinsi watu wetu wa kale walivyoletwa katika nchi hii, na za manabii wakuu wa kale.” Jinsi alivyopenda kusikia hadithi ya Eliya, na yule mwanamke Mshunami, pamoja na kufufuliwa kwa yule mtoto mchanga.

⁸ “Na jinsi mama yangu angeniambia, ‘Mpenzi, wakati mmoja, Mungu alikuwa pamoja na watu Wake, nao hawakupungukiwa na chochote.’ Halafu moja ya hadithi kuu, ambazo alizoea kuniambia ambazo zilikuwa za kustaaajabisha, ilikuwa ni jinsi ambavyo Mungu aliwalisha watu Wake wa kale, walipofikia mahali ambapo hawakuwa na chakula, hata hivyo wamesimama kwenye wajibu wao, wakiwa njiani kutoka—kutoka Misri kwenda Palestina.

⁹ “Ndipo wakati hawakuwa na chakula cha watoto wao, hawakuwa na kitu cha kusafiria, hakuna chakula tena, ndipo Mungu, Yehova, alinyesha mikate kutoka Mbinguni, tayari imepikwa, na kwa heshima, kwa Malaika Zake, akaitandaza ardhini kila usiku. Na jinsi watu wetu wangetoka nje na kuiokota hii, na ilikuwa imechovywa kwenye asali, na jinsi ingekuwa tamu, na kwa miaka arobaini bila kukoma, Yehova Mungu mkuu aliwalisha watu wetu, kwa sababu walikuwa kwenye wajibu wao.

¹⁰ “Basi sasa, ndugu zangu,” hapana shaka alisema hivi, ya kwamba “si ilileta hadithi hiyo upya kwangu, leo hii! Mtu huyu ana uhusiano na Yehova mahali fulani, kwa kuwa wakati aliposimama pale, basi nilipanda juu ya mwamba huo nyuma Yake, na kumwona akichukua hizo biskuti tano, angali anawalisha watu Wake wenye njaa. Kuna kitu fulani kumhusu

ambacho kina uhusiano na Mungu, Muumba, maana Mungu pekee...

¹¹ “Ningeshangaa, na kumwambia Mama, ‘Mungu angeweze kupandisha unga huo wote Mbinguni kuwalisha watu kwa miaka arobaini? Angeweza kupata wapi nyuki wa kutosha kutengeneza asali, kuichovya mana hiyo yote kwenye asali.’

“Naye mama yangu angesema, ‘Mwanangu, Mungu ni Muumba.’

¹² “Basi, ndugu, je, hilo halikuifanya mioyo yenu kuwaka moto leo, tulipomwona Mungu yuyo huyo, kwa mikono ya binadamu akichukua biskuti...? Nikapanda juu, na kumtazama Yeye alipokuwa akivunja mmoja, akawakabidhi, sikuliona likitukia wakati mmoja tu, nililiona likitukia zaidi ya mara elfu tano alasiri ya leo. Wakati mikono miwili ya kibinadamu ilipoumba mikate na samaki waliopikwa, na kulisha zaidi ya watu elfu tano, ninataka kuwahakikishia leo ya kwamba Mtu huyu ametoka kwa Mungu.”

¹³ Basi hapana shaka ilikuwa ni Simoni Petro, yeye alisema, “Miaka mingi iliyopita, wakati mimi na baba yangu...Na wengi wenu ninyi ndugu mlimjua baba yangu, mlijua ya kwamba alikuwa mtu wa dini, yeye alikuwa, shupavu zaidi wa dhehebu letu, alikuwa ni Farisayo. Tuliamini, kama Mafarisayo, ya kwamba Mungu anamaanisha kila Neno, hatuna budi kulidumisha Neno hilo. Baba yangu alikuwa mtu mashuhuri, mkali, aliamini ya kwamba Mungu alitimiza Neno Lake.

¹⁴ “Mara nyingi nimewazia tangu wakati huo, ambapo angenichukua jioni sana, wakati uvuvi wetu ulipokwisha, na kunyakua msuli wangu mdogo na kuuvuta juu, na kusema, ‘Simoni, una nguvu kama chuma,’ kisha akazipapasa nywele zangu kurudi nyuma na kunikumbatia kifua mwake, wakati ningempigapiga, na kuyaangalia macho yake yakififia kwa uzee, angesema, ‘Simoni, keti chini, ninataka kuzungumza nawe kidogo tu. Ninazeeka, Simoni, na siku moja itanibidi kuondoka, itanibidi kukuachia mtumbwi wangu, nyavu zangu. Wewe, pia, utavulia bahari hii, kama nilivyofanya. Nawe, pia, labda utahudhuria sinagogi lile lile nililohudhuria.

¹⁵ “Nami nimejaribu kuingiza katika maskini moyo wako wa Kiyahudi kwamba siku zote za maisha yangu, nimemtazamia Mtu ajaye, lakini Yeye anaonekana kuwa mbali sana sasa kuliko hapo awali, lakini labda, Yeye atakuja katika siku yako, Simoni. Na kama haji katika siku yako, wewe mfundishe mwanao. Kutakuwa na madoido mengi siku hizo.

¹⁶ “Lakini Simoni sikuzote kumbuka yale nabii aliyosema, kwa kuwa sisi kama Waisraeli tunawaamini manabii wetu, naye nabii Musa alisema ya kwamba Masihi huyu atakapokuja, ya kwamba Yeye angekuwa ni Nabii kama yeye. Sasa, Yeye hatakuwa mwelimishaji, hatakuwa mwanatheolojia fulani

mashuhuri, bali atakuwa ni Nabii, kwa sababu Musa alisema, “Bwana, Mungu wenu, atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Nanyi kumbukeni mtakapomwona Masihi huyu akiya, hiyo itakuwa ndiyo ishara kwamba ni Yeye, kwa sababu Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii, Yeye atakuwa ni Mungu katika mfano wa nabii, na kwa hilo mtajua.’

¹⁷ “Basi wakati ndugu yangu, Andrea, aliposhuka kwenda kwenye mikutano hii na kuniambia ya kwamba kulikuwa na Mponyaji kutoka Galilaya, akiwaponya wagonjwa kwa maombi, loo, kamwe sikuwazia sana juu yake. Basi akanishawishi kushuka niende nikamsikilize Huyu aitwaye Yesu wa Nazareti. Andrea alikuwa tayari amemwamini Yeye kama Masihi, lakini kwangu mimi, nilishikilia nyavu zangu za samaki.

¹⁸ “Ndipo basi, siku moja, nikahudhuria huo mkutano. Ndipo nilipoacha mashua yangu na kushuka ufukoni mahali alipokuwa, na kwenda mbele Zake, pasipo Yeye kunijua, macho Yake yaligeuka kama nuru, yakionekana kuchunguza kila kona ya nafsi yangu, na kuniambia, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’

¹⁹ “Ndipo mafundisho yote ya baba yangu yakaangaza mbele yangu, kweli huyu alikuwa ndiye yule Masihi, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii, si kwamba tu alinijua kwa jina, bali alimjua yule baba yangu mzee mtauwa, kwa kuwa Yeye alisema, ‘Wewe ni mwana wa Yona.’ Tangu siku hiyo, nikamfuata bila shaka lolote akilini mwangu. Haidhuru ulimwengu unasema nini juu Yake, yale watu wetu wasemayo, kwangu mimi, Yeye, tangu saa hiyo, Yeye amekuwa ndiye Masihi.”

²⁰ Yohana akasema, “Nilipomwona, kutoka kwenye hadithi ya Biblia, akijihusisha Mwenyewe leo na kuumba mkate na samaki, Ninajua ilibidi awe ndiye Masihi yule, hana budi kuwa.”

²¹ Ndipo nyuma kabisa, ningeamini, kuelekea kwenye shetri ya hiyo mashua, hiyo mashua ilikuwa ikielea wakati huu, kwa sababu machweo yalikuwa yakiingia, nao walikuwa, kile ambacho tungekiita leo, wakipumzika kutokana na kuvuta makasia yao kwa nguvu, hapana shaka ilikuwa ni Filipo aliyesema, “Ndugu, laiti mngalikuwa pamoja nami. Baada ya mimi kumwona Yeye siku hiyo, akisimama pale na kukwambia, Simoni ya kwamba jina lako lilikuwa ni *Simoni*, Naye akalibadilisha likawa *Petro*, ambalo tunakuwa sasa, akazungumza juu ya baba yako, ambaye nilimjua, nilikuwa nimeshawishika sana hata nilitaka kumwambia kila mtu.”

²² Na, mwajua, enyi marafiki, kusimama katika maskini mchezo wetu wa kuigiza, kuna jambo fulani kulihusu, mara unaposhawishika kwamba ni kweli, huwezi kutulia, huna budi kumwambia mtu fulani habari zake. Kuna kitu ambacho kabisa huwezi kutulia kukihusu, ni Uzima, nawe unataka kila mtu ajue.

²³ Naye akasema, “Unajua, nilikuwa na rafiki, ndugu yetu sasa, mpendwa katika Bwana, Nathanaeli, naye alikuwa umbali wa maili kumi na tano kutoka mahali ibada zilikuwa zikiendelea, nami nikaenda kwa miguu kuuzunguka mlima. Hatimaye, nikafika nyumbani kwake, na kubisha mlangoni, naye mke wake mpendwa akaja mlangoni, nami nikauliza mahali alipo Nathanaeli.

“Naye akasema, ‘Filipo, anatembea bustanini.’

²⁴ “Basi nikaenda bustanini, ndipo nikasikia mtu fulani kule chini ya mti, naye alikuwa akiomba hivi: ‘Loo, Yehova Mkuu, tumetamani na kutamani wakati ambapo Wewe ungetutumia ukombozi. Hivi hutatutumia M—Mkombozi sasa tafadhali? Kama vile ulivyomtuma Musa wakati watu Wako walipokuwa katika shida, ututumie msaada sasa.’

²⁵ “Nami nilivutiwa sana kumwambia ya kwamba Msaada umekuja, hata nikasahau kusema mengi sana alipoondoka magotini mwake, nikasema, ‘Njoo, umwone Yule tuliyemwona, Masihi, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu!’ Kamwe nisingeweza kuchukua wakati kumwambia jambo lingine lolote. Lilikuwa limeingia moyoni mwangu *sana*, ilinibidi tu kulifungulia litoke.”

²⁶ Hivyo ndivyo ilivyo wakati Mungu anapoushika moyo ulioshawishika kweli, kamwe huwezi kutulia, huna budi kumwambia mtu, huwezi kulificha hili. Kuwasha mshumaa na kuuweka chini ya kikapu hakufai kitu, huna budi kuiacha Nuru yako iangaze.

²⁷ Naye akaja upesi kwenye hoja yenyewe, na kusema, “‘Njoo, umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti.’ Na bila shaka, ninyi ndugu mnajua ya kwamba Nathanaeli daima alikuwa ni mwanatheolojia kwelikweli, basi akasema, ‘Sasa, ngoja kidogo, Filipo, nimekujua kwa miaka mingi, nami ni—nimekuwazia kuwa mtu mzuri, mwenye akili timamu, mwenye busara. Lakini sasa, usiniambie umeingilia namna fulani ya ulokole, ama ukaingia wazimu, na umepotelea hapa nje pamoja na Nabii mlakole fulani, *anavyojiita*! Kama kungekuweko na Masihi yeyote, hivi hudhanii ya kwamba kuhani mkuu angejua jambo hilo? Hivi hudhanii ya kwamba Yeye angekuja kwenye dhehebu letu, na kutwambia habari zake?’”

²⁸ Lakini mnajua, kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo siku hizi. Kitu ambacho Mungu anatumia, hakina budi kuja kwenye dhehebu letu, la sivyo si—si cha kweli kabisa. Lakini Mungu kwa kawaida hukituma nje ya kila dhehebu, na kukichanganyisha kikosi chote, kwa wale wanaotazamia na kungojea kitu fulani.

²⁹ Kwa hiyo, akasema, “Nilimnukulia hiyo hadithi, naye akasema, ‘Sasa, Filipo, unajua hakuna neno jema lingeweza kutoka Nazareti.’”

Naye Filipo, nafikiri, alimpa jibu zuri sana nililopata kusikia, “Usikae nyumbani na kukosoa, njoo, ujionee mwenyewe.”

³⁰ Hilo ni jambo jema, wakati watu wanaposema ya kwamba Roho Mtakatifu hatembezi miongoni mwa watu siku hizi, kwamba huo ni mhemuko, nafikiri jibu zuri sana ni, “Njoo, ujionee mwenyewe. Ujionee yanayotukia.”

³¹ Wakati watu wa matabaka yote ya maisha, waovu, walevi, viruka njia, na kadhalika, wanaponyoshwa, na kusafishwa kwa Damu ya Yesu Kristo na kufanywa watakatifu, hilo linahitaji zaidi ya saikolojia, ama—ama theolojia ya kibinadamu, ama, linahitaji nguvu, nguvu za kuzaliwa upya za Roho Mtakatifu kuibadilisha nafsi ya mtu, nia yake, njia yake ya kuishi.

³² Naye akasema, “Nathanaeli akajiandaa, ndugu zangu.” Nao maskini ule mtumbwi, bila shaka, umechukuliwa na mkondo, kukiingia giza. Naye akasema, “Nathanaeli akapitia mashambani, nami nikamwambia habari zako, Simoni. Na kumwambia ya kwamba alikukumbuka, jinsi tulivyonunua samaki kwako mara kwa mara, na hata kwa baba yako, ya kwamba hukuwa mtu mwenye elimu, hata usingeweza kutia sahihi risiti ya hao samaki, bali kwamba ulijua ya kutosha kujua ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu ulijua Mungu alikuwa ameahidi hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi, na ukaiamini.

³³ “Ba—basi nilipomleta Mbele za Bwana wetu aliyebarikiwa, nami nikaenda kwenye mstari mahali alipokuwa akiwaombea wagonjwa, mara alipouangalia uso wa Nathanaeli, ilijirudia tena, Yeye alisema, ‘Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!’

³⁴ “Nayo ilimshangaza Nathanaeli hivi kwamba, alisema, ‘Rabi, ulinijua lini Wewe?’” Kwa maneno mengine, “Hujawahi kuniona maishani Mwako. Ulijuaje kwamba nilikuwa Mwisraeli?”

³⁵ Sasa, Yeye asingejua hilo kwa jinsi alivyovalia, kwa sababu Wapalestina huvalia kwa njia inayofanana sana, nao walikuwa kwa namna fulani watu weusi, nao walikuwa na ndevu, na vilemba vyao, na majoho yao, na kadhalika.

“Kwa hiyo, Yeye alijua alikuwa Mwisraeli, ‘Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!’

“Akasema, ‘Ulinijua lini Wewe, Rabi?’

“Akasema, ‘Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’

³⁶ “Hilo lilitosha. Tangu siku hiyo na kuendelea, ndugu, nyote mnajua ya kwamba Nathanaeli amekuwa mwaminio hodari, kwa sababu alianguka kifudifudi, akasema, ‘Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’

³⁷ “Ishara Zake na maajabu yake yametushangaza. Nasi tunajua kwa matendo Yake, na yale asemayo, kwa sababu yale asemayo yanatimia. Yeye si mtu anayezungumza tu juu ya jambo fulani, Yeye ni Mtu anayeleta kile anachozungumzia.” Jinsi tulivyo na furaha siku hizi, kwamba Yeye angali anafanya yale anayonena katika Neno Lake!

³⁸ Nimeshika Kurani kwa mkono mmoja, na Biblia katika huo mwingine mbele ya maelfu mara maelfu ya Waislamu, na kusema, “Vyote viwili haviwezi kuwa sahihi, kwa sababu vinapingana. Basi hebu Yule atakayenena, na kutenda, na kufanya yale aliyosema angefanya, basi huyo awe Ndiye Mungu, hebu Yule anayelitimiza Neno Lake. Kwa kuwa kama Yeye aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu.

³⁹ “Hawezi kubadilika, kwa sababu Yeye ni—Yeye ni asiyepatikana na mauti, Naye hana kikomo, anajua yote, yuko kila mahali, na Yeye hawezi kubadilika, Yeye ni Mungu asiyeweza kukosea, na usiku wa leo yu kadiri alivyokuwa wakati huo, na daima atakuwa vivyo hivyo. Kamwe hawezi kubadilika kutoka kile alichu Yeye, maana Yeye ni mkamilifu, kwa hiyo, unaweza kuwa na hakika ya kwamba anaposema jambo lolote katika Neno Lake, yaweke maisha yako kwamba hiyo ni kweli.”

⁴⁰ Kwa sababu, kama Mungu akiwahi kuitwa jukwaani kutoa uamuzi, uamuzi Wake ni mkamilifu, kamwe hawezi kurudi katika wakati mwingine, na kusema, “Nilikosea.” Kwa sababu, tunaweza kufanya hivyo, kwa sababu sisi tuna kikomo, nasi hukosea, bali Yeye hana kikomo, wala hawezi kukosea. Kwa hiyo basi kama Mungu aliitwa jukwaani kwa ajili ya mtu aliyepotea katika bustani ya Edeni, alifanya maandalizi kwa ajili ya mtu huyo kuokolewa, akamwoko, basi kwa msingi uo huo, maandalizi yale yale, katika damu iliyomwagika ya mtu asiye na hatia, Mungu atamwoko kila mwenye dhambi amjiaye.

⁴¹ Kama mtu akimjia akiwa mgonjwa, naye alitaka uponyaji, alikuwa amepita msaada wa madaktari na kadhalika, ndipo Mungu akaitwa jukwaani, Naye akamponya mtu huyo juu ya msingi wa imani yake Kwake, wakati mtu mwingine anapoitwa, Mungu atatenda vivyo hivyo, asipotenda hivyo, basi alikosea alipotenda mara ya kwanza. Mnaona? Kwa hiyo Yeye hawezi kuwa Mponyaji mara moja, wala asiwe Mponyaji tena. Hawezi kuwa Mungu wa miujiza siku moja, na asiwe Mungu wa miujiza kesho yake, kwa kuwa Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yeye angali ni Mungu.

⁴² Na kama utachukua msimamo mzuri wa kiakili kuhusu ahadi yoyote. . . Unapoisoma katika Biblia, ni kweli, haijalishi ni wangapi wanaojaribu kuiweka kwenye wakati mwingine, “Iko katika wakati uliopita, ama wakati wa siku za usoni.” Kamwe Yeye hakutangaza ya kwamba alikuwa *Nilikuwa*, Yeye ni *MIMI NIKO*, daima.

⁴³ Sasa, hapana shaka ilikuwa yapata wakati huo ambapo Andrea, akiketi karibu na Simoni, kama sisi kwa jumla, kama usiku wa leo, ningesema, “Ningetaka kusikia ushuhuda wa mtu fulani aliyeokolewa kwa neema Yake,” mbona, ingetubidi kuisimamisha hii ibada saa nane usiku, kila mtu anataka kusema yale wanayojua kumhusu, kama umewahi kumjua.

⁴⁴ Loo, kuna jambo fulani kulihusu ambapo unataka kumwambia kila mtu, kwa sababu unajua unachozungumzia, si imani fulani nusu nusu iliyochanganyikana katika jambo fulani, ni kitu fulani wakati umempokea Kristo kama Mwokozi wako, na Roho Mtakatifu ameingia maishani mwako, unajua jambo fulani lilitukia, kwa kuwa ulikuwa hapo, na lilitendeka kwako wewe. Kama umewahi kuponywa kwa nguvu za Mungu, hakuna kitu ulimwenguni kingaliweza kuondoa hilo akilini mwako, wasingeweza kulielezea vinginevyo, kwa sababu wewe *unajua*.

⁴⁵ Nafikiri kila mtu anayetoka kwenda kuihubiri Injili, hawapaswi kamwe kwenda mpaka wawe na tukio la kibinafsi la ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninaamini hiyo ilikuwa ndiyo sifa ambayo Yesu aliwapa, “Ngojeni katika mji wa Yerusalemu, hata mvikwe uwezo, ndipo mtakapokuwa mashahidi Wangu, katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria; na Shreveport, Louisiana,” kama ingesomeka namna hiyo. Natumaini hilo halisikiki la kukufuru, bali mnajua ninalomaanisha nalo.

⁴⁶ Hakuna mtu, haijalishi umeelimika vizuri jinsi gani, jinsi ulivyo hodari katika Biblia, ibilisi ni mwerevu maradufu kuliko ulivyo wewe. Naam, bwana. Angeweza kulipindua na kukufanya uonekane kama Ned katika *Msomaji Wa Kwanza*, akitaka kufanya hivyo, bila shaka anaweza. Lakini kama umewahi kupata tukio, na kukutana na Mungu uso kwa uso, hakuna pepo wa kutosha kuzimuni kuiondoa kwako, kwa sababu *unajua* unachozungumzia.

⁴⁷ Musa katika mafunzo yake yote, hata angeweza kuwafundisha Wamisri theolojia, hakurudi Misri, wala Mungu hakumtuma akaimarishe hisabati zake, ama mbinu zake za vita, kamwe hakumtuma huko chini kusomea digrii nyingine chuoni, bali alikutana naye karibu na kichaka kilichowaka moto kwenye mchanga mtakatifu nyuma ya jangwa, na kumpa tukio ambalo usingeweza kulielezea vinginevyo kwake.

⁴⁸ Pamoja na theolojia yake yote, alikosea, naye alikuwa akimkimbia Mungu, lakini alipokutana na Mungu uso kwa uso, jambo fulani lilimpata hata akawa tayari kurudi Misri. Haidhuru hali ya mambo ilikuwaje, alikuwa akienda zake, kwa sababu alikuwa na tukio, alijua alichokuwa anazungumzia. Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mwaminio aliyempokea Roho Mtakatifu.

⁴⁹ Kwa hiyo, ningesema usiku wa leo, hao wanafunzi katika meli hiyo ndogo, ilikuwa kama vile tungekuwa hapa usiku wa

leo, sisi sote tunataka kumwambia mtu fulani, kutoa tukio, tungetaka kulisimulia kinagaubaga, hivyo ndivyo walivyokuwa.

⁵⁰ Kwa hiyo hapana shaka Andrea ndiye aliyefuata, asingeweza kutulia zaidi. Walikuwa tayari wamevuta makasia katika mtumbwi, na labda ulikuwa ukielea wakati huo, giza lilikuwa likiingia, naye akasema, “Ndugu, sote tunganeme nini juu ya jambo hili? Je, mnakumbuka wakati tulipokuwa tukienda Yeriko, Naye akasema alikuwa na haja kupitia Samaria? Nasi tukashangaa, ‘Kwa nini azunguke aende kwa hao Wasamaria?’

⁵¹ “Lakini alipofika mjini, basi, aliketi kisimani, na kututuma mjini kununua chakula. Basi tuliporudi, mnakumbuka, sisi sote ni mashahidi wa jambo hili, tulikaribia na kumsikia Yeye akinena? Basi hili lilitushangaza sote, Bwana wetu angezungumza na mwanamke kama aliyekuwa akizungumza Naye. Lakini tulisikia mazungumzo tulipoingia tukasikiliza nyuma ya kichaka, au, nyuma ya ukuta, wakati alipomwambia, kasema, ‘Mwanamke, nipe maji ninywe.’

⁵² “Naye akasema, ‘Si kawaida kwenu Wayahudi, kumwomba Msamaria, mwanamke Msamaria fadhili. Tuna ubaguzi, hatuna uhusiano sisi kwa sisi.’

⁵³ “Lakini Yeye akamwambia, ‘Lakini kama ungalijua ni Nani anayesema nawe!’” Loo, hilo hapo, “Kama ungalijua ni Nani aliyekuwa akisema nawe!”

⁵⁴ Nina hakika kama kila mwenye dhambi hapa ndani, anahisi ule Uwepo na mazingira haya ya kuketi pamoja usiku wa leo katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, na *hisia* hiyo ndogo inayokwambia, “Laiti ungalijua ni Nani aliyekuwa akisema nawe! Unapaswa kuwa na ujuzi huu.”

⁵⁵ “Labda watu hao wako sahihi, kama,” unawazia moyoni mwako, “huyo ni Mungu anayenena.” Laiti ungalijua tu Huyo alikuwa ni Nani!

⁵⁶ “‘Kama ungalijua Huyo alikuwa ni Nani aliyekuwa akinena, ungeniomba Mimi maji unywe, nami ningekupa Maji usiyokuja hapa kuteka.’

“Naye akasema, ‘Kisima ni kirefu, wala huna kitu cha kuchotea,’ na kadhalika.

“Lakini Yeye alisema, ‘Maji ninayotoa ni Uzima unaobubujika, Uzima wa milele.’

⁵⁷ “Ndipo basi swali likatokea kupitia mjadala wa kidini, mahali unapopaswa kwenda kanisani. Kasema, ‘Mnasema, inatupasa sote kwenda Yerusalemu, huku baba yetu, Yakobo, alichimba kisima hiki, na kuwaruhusu mifugo wake kukinywea, na jamaa yake, na—nasi tunaabudu katika mlima huu, na Wewe unasema huko Yerusalemu.’

⁵⁸ “Ndipo upesi Yeye akasema, ‘Si katika mlima huu, wala huko Yerusalemu, bali Mungu ni Roho, hao wamwabuduo Yeye

imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli, Roho na kweli.' Ndipo akasema basi, alipowasiliana na roho yake na kujua shida yake ilikuwa ni nini, alisema, 'Nenda kamwite mumeo, mje hapa.'" [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

"U nani Wewe?"

"Naye akasema, 'Mimi ninayesema nawe Ndiye.'

⁵⁹ "Hakuna mengine yaliyohitajika kusemwa, alishawishika ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa na Agano la Kale." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "Akasahau mambo yote ya ulimwengu, hata akaacha mtungi wake wa maji umewekwa pale, akakimbia mjini, na kusema, 'Njoni, mwone Mtu, ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?' Ndipo watu wa huo mji wakamwamini, kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke."

⁶⁰ Sijui kama watu wa Shreveport wangemwamini usiku wa leo, kama Yeye, akiwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angekuja kwenye Maskani ya Uzima, na angefanya mambo aliyofanya wakati huo. Sijui kama tunganishawishika sana, hata tungeweza kumwambia jirani yetu, na kuwaambia watu, "Njoni, mwone Mtu, Ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?"

⁶¹ Nashangaa basi, kama ingesemwa basi kwamba "Hakika Huyu ndiye Masihi. Ni huyu Roho Mtakatifu ambaye wanazungumza habari zake, ambaye ulimwengu unamwita mlokole, imethibitishwa kuwa ni Masihi yeye yule, pamoja na ishara zile zile, na maajabu yale yale, na nguvu zile zile, na ukombozi ule ule."

⁶² Sijui kama ingeweza kusemwa namna hiyo. Ingekuwa ndio ulinzi mkubwa zaidi kuliko kinga zote za bomu mngeweza kujenga. Hiyo ni kweli. Ingekuwa ni tukio la kunyakuliwa.

⁶³ Loo, wote walishawishika. Hapana shaka ilikuwa yapata wakati huo kukaingia giza, naye Shetani akawaona wakiwa peke yao, bila Yeye.

⁶⁴ Sasa, hilo tu ndilo ibilisi analotaka, ni kuona kanisa bila Kristo. Sijali jina lako ni nani, jinsi jina lako lilivyo katika herufi za dhahabu, "Sisi ni kanisa takatifu, sisi ni *hili*." Si kanisa takatifu, hakuna kitu kama kanisa takatifu, hakuna kitu kama milima mitakatifu, masalio matakatifu, ama hata watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya watu ndiye anayefanyiza sehemu hiyo *takatifu*, Roho Mtakatifu.

Unasema, "Loo, yeye ni mtu mtakatifu."

Yeye si mtu mtakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya mtu huyo.

⁶⁵ Sikuzote kwa namna fulani ninatofautiana na msemu, "Matendo ya mitume." Hayo si matendo ya mitume, hao walikuwa ni wanadamu, ilikuwa ni matendo ya Roho Mtakatifu *ndani* ya mitume, ndiyo yaliyoleta huo ushindi mkuu.

⁶⁶ Basi Shetani alipoona lile kanisa dogo bila Kristo, ndipo akasema, “Hii ndiyo nafasi yangu. Huu ndio wakati ambao nitawafundisha jinsi ya kunikufuru!” Ndipo akaanza kupuliza kwa pumzi yake, dhoruba chini kwenye bahari.

⁶⁷ Nao maskini ule mtumbwi ulikuwa karibu kuzama, labda, huko Galilaya, mawimbi yalikuwa mazito sana karibu wazame chini. Na labda, kwenye kila wimbi linalometameta, na kila radi, wakati ilipomulika, ibilisi angecheka huko nje, na kusema, “Nimewapata sasa, kwa sababu wameondoka bila yeye.”

⁶⁸ Nilisema jambo fulani kuhusu hilo wakati mmoja, ndipo mtu fulani akanisahihisha baadaye, kasema, “Lakini, Ndugu Branham, Yeye aliwashurutisha waondoke bila Yeye.”

Nikasema, “Naam, lakini walikosea kwa kufanya hivyo.” Nikasema, “Wakati Eliya na Elisha, ambao walikuwa ni mifano, Kristo kwa Kanisa . . .”

⁶⁹ Elisha alichukua sehemu maradufu ya Roho, “Mambo haya nifanyayo mtayafanya, na makubwa kuliko haya mtayafanya.” Wakati lile joho lililokuwa juu Yake, Roho Mtakatifu aliyekuwa juu Yake, anapolishukia Kanisa, maana Yeye alikuwa ni Mtu mmoja tu, Kanisa ni la ulimwenguni kote, “Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.” Naye Elisha alijua zaidi juu ya jambo hilo, akiwa ni nabii, kuliko kanisa linavyojua siku hizi.

⁷⁰ Eliya akasema, walipokuwa pamoja, akasema, “Wewe kaa hapa, Bwana ameniita kule. Ninapanda kwenda kwenye shule ya manabii.”

⁷¹ Lakini Elisha, kama vile Kanisa linavyopaswa kuwa leo, “Kama Bwana Mungu aishivyo, sitakuacha.” Kwa kuwa alikuwa na ku—kusudi niani mwake, na nia zake hakika zilikuwa sahihi.

⁷² Alipofika kwenye shule ya manabii, alisema, “Wewe kaa hapa, Bwana ameniita niende Yordani.”

⁷³ Akasema, “Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha.” Asingeweza kumwacha, alikaa moja kwa moja karibu naye, macho yote mawili yakiwa juu yake, akimshikilia.

⁷⁴ Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kufanya siku hizi, haijalishi kijacho wala kiendacho, mshikilie Yeye. Kanisa likipoa, haijalishi ni kitu gani kinachotukia, shikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Shikilia Kalvari, na ukae hapo. Hiyo ndiyo njia ya kupata kitu kutoka kwa Mungu. Ushikilie, usiache ibilisi akuondoshe.

Hao wanafunzi wanapaswa kusema, “Uendako, ninaenda.”

⁷⁵ Kama vile Ruthu kwa Naomi, yule Mmoabu, “Watu wako na wawe wangu; utakapofia, nitakufa; utakapozikwa, nitazika; alipo Mungu wako, mimi, huyo atakuwa Mungu wangu. Nitakaa pamoja nawe.”

⁷⁶ Hivyo ndivyo alivyomvutia Boazi; hivyo ndivyo Kanisa linavyomvutia Kristo. Haidhuru, yale ulimwengu utakayo kusema. Waseme, “Umeingia wazimu, umefanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo*,” kaa pamoja na Kristo, mshikilie, dumu nalo.

⁷⁷ Shetani aliona hilo, ninaamini analiona leo. Yeye alitubariki, na loo, jamani, wakati Pentekoste ilipoanza kuanguka kwa mara ya kwanza, miaka arobaini iliyopita, ama zaidi, ni mikutano mikuu jinsi gani tuliyoukuwa nayo! Lakini mnajua, tuliingilia miradi *mikubwa sana* ya ujenzi, ilitubidi kuwa na shule, na seminari, na kadhalika, kwa ajili ya wachungaji wetu, ili wawe na hotuba zenye ufasaha zaidi, kuwafundisha kuwa madaktari, na kuwafanya waangalizi wakuu, na madaktari wa uungu, na majina haya yote makubwa. Shetani aliona hayo yote, na sasa bahari imechafuka.

⁷⁸ Anaona kanisa limeingia kwenye mradi mkubwa wa ujenzi, ama namna fulani ya kitu kikubwa mno, namna hiyo, kisha likaondoka bila Yeye, *wakijipamba*, wagumu. Tunachohitaji leo ni uamsho wa mtindo wa kale, nguvu za Roho Mtakatifu tena, kurudi kanisani. Mungu anajua tunahitaji hizo katika makanisa yote, bali tunapotoka kwa *mapambo*, tunataka kutenda kama makanisa mengine, hayo mengine. . .

⁷⁹ Ninyi ni watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, waliotengwa na kuitwa watoke. Mungu anajua ya kwamba tunahitaji kanisa lirudi pamoja na Roho Mtakatifu tena. Hata kama ilitulazimu kufanya mambo, haidhuru inatubidi kufanya nini, kamwe tusimwache Yeye, kaeni pamoja Naye.

⁸⁰ Wakati mwingine inamaanisha mengi, wakati mwingine inakugharimu kitu. Chochote ambacho hakikugharimu kitu, hakifai kuwa nacho. Mambo yote makuu hayana budi kulipiwa. Sababu ya sisi kuabudu siku hizi, uhuru wa dini katika Siku hii ya Shukrani, huu uligharimu damu ya Wamarekani wengi, mamilioni yao, una thamani fulani. Na kama una thamani fulani, unastahili kufiwa. Nayo dini hii tuliyo nayo, huyu Roho Mtakatifu wa Kipentekoste ambaye ametushukia, ameturudishia Yesu Kristo aliyefufuka aliye hai baada ya miaka elfu moja mia tisa anastahili wakati wetu wote, na jitihada zetu, na kila kitu tufanyacho, anastahili yote kwetu.

Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,
 (alisema Fanny Crosby)
 Zaidi ya maisha kwangu,
 Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?
 Au ni nani Mbinguni ila Wewe?
 Usinipite, Ee Mwokozi mpole.

Hakika, tunahitaji kurudi, na kumshikilia Yeye.

⁸¹ Wanafunzi waliona ya kwamba matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Karibu tuko mahali hapo leo. UN zetu zote

kuu, nzuri za dola milioni moja, na UN za makanisa, na majengo ya makanisa ya dola milioni moja, na kadhalika namna hiyo, bomu moja dogo la atomiki litafagilia mbali kitu hicho chote. Hiyo ni kweli. “Lakini loo, njoni mnunue Kwangu,” alisema Yesu, “Mafuta, divai, dhahabu iliyosafishwa kwa Moto.” Wakati ulimwengu wote unawaka moto, ninataka kitu kitakachosimama wakati huo, ninataka kitu:

Mwamba wa Miaka, uliopasuliwa kwa ajili
yangu,
Jalia nijifiche Kwako.

Jalia nijifiche Kwako.

⁸² Charles Wesley, ninaamini, wakati alipokuwa akitembea, nayo dhoruba ikija, ndipo ndege mdogo akaruka kifuani mwake. Alikuwa akijaribu kupata uvuvio atunge wimbo. Naye akampeleka kwenye maskini kibanda chake kidogo, na kumshikilia mpaka dhoruba zikapita. Alipotoka, alimshikilia kidoleni mwake, naye akaruka, ndipo akaandika wimbo huo. Nifiche katika Mwamba wa Miaka.

⁸³ Sasa, halafu wakati alipoona...walipoona hilo, Shetani alianza kupuliza pumzi yake ya sumu, naye akaanza kuwafadhaisha. Ile meli ndogo ilikuwa karibu kuangamia.

⁸⁴ Nami nashangaa usiku wa leo katika ganda letu dogo, tunaposafiri juu ya bahari adhimu ya maisha, kama labda, Shetani amevuruga safari yako, ameweka kansa juu yako, akakupa kuupenda ulimwengu, umemwacha Mungu, amekuvuruga mahali fulani, shida imeingia, matumaini yote ya kuishi tena yamekwisha.

⁸⁵ Lakini unajua, kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa, Yesu hakuwa ameenda mbali sana. Ninaamini alipanda kilima kirefu zaidi kilichokuwako nchini, kwa hiyo Yeye, kadiri unavyopanda juu ndivyo unavyoweza kuona mbali, alipanda juu ya kilima kusudi aweze kuwaangalia. Wakati wote shida ilipokuwa ikija Yeye alikuwa ameketi pale akiwaangalia.

⁸⁶ Nami nawaambia, wakati Yeye, walipomwua katika mji wa Yerusalemu na kumzika katika kaburi la kuazimwa, lakini kwenye asubuhi ya Pasaka alipofufuka, alianza kupanda. Akapanda kupita mwezi, nyota, hata akaketi mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, “Nalo jicho Lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia,” alisema mshairi.

⁸⁷ Nami ninaona siku hii ikikaribia wakati nabii alisema, “Inakuja siku katika siku hizi za mwisho, ambayo haitakuwa usiku wala mchana, utusitisi tu, lakini,” akasema, “itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

⁸⁸ Sasa nuru, jua huchomoza mashariki, linatua magharibi, j-u-a; na M-w-a-n-a pia alikuja mashariki, kwa watu wa Mashariki, akaangazia uamsho wa Kipentekoste, ishara na

maajabu ya kufufuka Kwake yalionekana miongoni mwao, kazi alizofanya, walizifanya pia, Yeye aliwaambia hivyo. Yohana Mtakatifu 14:7, ninaamini ndiyo, Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” *ninyi*, Kanisa, mwaminio, “mtaniona Mimi.”

⁸⁹ Aliahidi ya kwamba atakuwa pamoja nao daima, hata ukamilifu wa dahari. “Kamwe sitawaacha wala kuwapungukia. Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili.”

Umbali gani?

“Ulimwenguni kote.”

Kwa akina nani?

“Kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yeye angali ni Kristo yeye yule.

⁹⁰ Ndipo ikaja siku basi, kumekuwa na siku ikipita, kipindi cha wakati, siku yenye utusitusi, kama inavyokuwa huku chini Louisiana na Arkansas, kote nchini, ukungu, hatuwezi kuona jua, hata hivyo tunajua jua linatoa nuru. Tumekuwa na Nuru ya kutosha kuunda madhehebu, tumekuwa na Nuru ya kutosha kujiunga na kanisa, tumekuwa na Nuru ya kutosha kumkubali Yeye kama Mwokozi, lakini nabii alisema Mwana angeangaza katika siku za mwisho, katika saa za mwisho, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

⁹¹ Sasa jua linatua, liliwazukia watu wa Mashariki, nalo linatua juu ya watu wa Magharibi. Na jua lile lile lililoangazia mashariki, hutua magharibi; linavyochomoza mashariki, linatua magharibi, jua lile lile. Nasi tunaishi katika siku za mwisho, ambapo siku imefikia ambapo Mwana yeye yule, M-w-a-n-a yeye yule, nguvu zile zile za Roho Mtakatifu zinawashukia watu wa Magharibi kama zilivyowashukia watu wa Mashariki, zikionyesha Nuru ile ile ya Injili, si theolojia, si madhehebu ya kanisa, si kujiunga, bali nguvu fulani, ushahidi wa ufufuo, na nguvu Zake za uponyaji, na ishara na maajabu Yake kuwa miongoni mwao katika siku za mwisho. “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Tuko hapa, tumewasili.

⁹² Mashariki imeenda mbali sana, ustaarabu umetoka mashariki ukienda magharibi, tuko kwenye Pwani ya Magharibi sasa, tukienda mbele zaidi, tutarudi mashariki tena. Tuko katika wakati wa mwisho, mitumbwi inaporomoka, ustaarabu unaporomoka, makanisa yanavunjika.

Wimbo ule ulioandikwa miaka mingi iliyopita:

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,

Hilo ni taifa sasa, linalojitawala, Israeli wako katika nchi ya uenyeyi wao.

Ishara ambazo manabii walitabiri;

Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu nyingi;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

⁹³ Huu sio wakati wa kupoa, huu ni wakati wa kushika moto, huu ni wakati wa mkutano wa maombi. Tunaingia kwenye wakati wa Laodikia. Ni wakati wa kumjia Mungu, wakati wa uamsho.

⁹⁴ Nilipokutana na Ndugu Lyle kule nyuma muda mfupi uliopita, naye akasema, “Ndugu Branham, kuna ishara ya uamsho katika kila mkutano hapa sasa,” Mungu ashukuriwe, hilo ndilo tunalotaka. “Ee Bwana, tuma zile nguvu sasa hivi.” Tunataka uamsho, sio kujiunga na makanisa, bali uamsho. Kufufua kile kilicho ndani yetu.

⁹⁵ Wale wanafunzi, hebu tusifanye kosa lile lile walilofanya. Wakati matumaini yote yalikuwa yamekwisha, walidhani wasingeweza kuwa na uamsho tena, kamwe hawangemwona Yesu maishani tena, wakati wakiwa hapa, lakini papo hapo kwenye saa yenye giza kuliko zote, wakati matumaini yote yalipokuwa yamewisha, Yeye aliwajia akienda kwa miguu juu ya maji.

⁹⁶ Yeye anakuja kwetu leo, akienda kwa miguu juu ya maji, Ufunuo 17:15 inasema, “Maji uliyoyaona, ni makutano na wingi wa watu.”

⁹⁷ Tunapomwona Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliyefufuka akitembea, akifanya kazi miongoni mwa watu Wake, akifanya mambo yale yale aliyofanya huko nyuma, hao wanafunzi, na kadhalika, walimtambua Yeye kuwa ni Masihi, ilichochea mioyo yao, inapaswa kuichochea mioyo yetu. Lakini hebu tusifanye kosa walilofanya kwenye bahari ya Galilaya usiku huo, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwaokoa, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwakomboa, walikiogopa, nao walidhani kilikuwa ni mzuka. Hiyo ni kweli kabisa. Usituache tufanye kosa lilo hilo.

⁹⁸ Kama akipenda, Yeye aliyepo kila mahali kwa kuwa mwenye nguvu zote, Yeye anayejua na kusikia sasa, kama Yeye atatembea miongoni mwa watu Wake usiku wa leo, kama atafanya mambo aliyofanya wakati huo, ili mpate kuona ya kwamba Injili hii tunayohubiri, si theolojia ya kujibunia, si nadharia ya kujibunia, bali ni nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo zikitembea miongoni mwa watu Wake, msiliogope, ndilo jambo pekee linaloweza kuwasaidia.

⁹⁹ Mnapowasikia watu wakisema, “Siku za miujiza zimepita, Roho Mtakatifu si kama alivyokuwa,” msiamini hilo. Kristo alifufuka katika wafu, Yeye yu hai usiku wa leo. Maombi yangu ni kwamba Yeye atatembea miongoni mwetu usiku wa leo, na kutenda, na kuwaponya wagonjwa, na kufanya mambo yale yale

aliyofanya wakati huo, akituonyesha ya kwamba Yeye yu pamoja nasi, ya kwamba Yeye ni yule yule. “Msiogope, ni Mimi.”

Loo, mwasema, “Mtu huyo ana akili thabiti. Mwanamke huyo. . .”

¹⁰⁰ Si hivyo, si saikolojia, watu hawa wote ni watu wa kawaida. Na haidhuru Kristo angenitia mafuta kiasi gani, hana budi kukutia mafuta, pia, kuliadini. “Miujiiza mingi asingeweza kufanya kwa sababu ya kutokuadini kwao katika mji Wake Mwenyewe.” Hana budi kuwatia mafuta jinsi anavyonitia mafuta. Kama atakuja usiku wa leo, na kututia mafuta sisi sote, loo, hilo ndilo ninalotaka kuona, ni upako wa Roho Mtakatifu Kanisani, juu ya watu, Kristo. Ndipo watu watasema. . .

¹⁰¹ Paulo alisema, yule Mtakatifu Paulo mashuhuri alisema, “Ikiwa nyote miongoni mwenu mkinena kwa lugha, wala hakuna anayefasiri, kama mtu mjianga akiingia, basi aliye mjianga atatoka na kusema, ‘Ninyi nyote mna wazimu.’” Kwa maneno mengine, *kichaa*, nyote mkinena kwa lugha, wala hakuna wa kufasiri. Lakini kasema, “Akiwepo nabii, naye mwenye kutabiri awajulishe siri ya moyo, basi wote wataanguka chini, na kusema, ‘Hakika, Mungu yu pamoja nanyi.’” Kwa kuwa daima imekuwa kwa watu wa Mungu, kwamba nabii, walijua hilo.

¹⁰² Biblia ilisema huko nyuma, Mungu alisema, “Akiwepo mtu miongoni mwenu aliye wa rohoni, ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake. Na yale asemayo, yakitimia, basi msikieni.” Hiyo ndiyo sababu Wayahudi wa siku hiyo watakuwa bila udhuru, maana waliona yale Musa aliyosema yakitimia katika Yesu Kristo; yale Isaya aliyosema, yale Agano la Kale liliyosema, yalithibitishwa katika Yesu Kristo, Naye alikuwa ni Nabii, Naye alisema kweli, na Mungu akaonyesha ishara Yake. Lakini bila shaka, tunajua ya kwamba iliwabidi kupofushwa, kwa sababu tusingekuwa na nafasi, bali walipofushwa kusudi tupate nafasi.

¹⁰³ Kwa hiyo kama kile Kisiki kilikuwa kitakatifu, nasi tuwe mizabibu iliyopandikizwa, afadhali tuangalie jinsi tunavyoenenda. Hebu tusiwe watoto wa usiku, hebu tutembe mchana. Na kama Roho Mtakatifu atakuja usiku wa leo, aliyemfua Yesu katika wafu, Yeye aliahidi, “Bado kitambo kidogo, na asiyeadini hataniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” na *mimi* ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari,” ule ukamilifu. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata mwisho wa ulimwengu. Na mambo nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya.”

¹⁰⁴ Hiyo si ni ahadi? Ni ahadi, lakini je, itafanya kazi? Jambo ndilo hilo. Kama hilo likitenda kazi, basi yote hufanya kazi kama Yeye anaweza kuthibitisha Yeye yu hai. Naye anaweza kuthibitisha Yeye yu hai kama utamruhusu alithibitisha ndani

yako, nami nimwache alithibitishe ndani yangu, kwamba, kwako, na wewe kwangu mimi, kwamba Yeye yu hai, basi Yeye anatembea miongoni mwa watu Wake usiku wa leo, katikati ya maji kama alivyofanya wakati huo. Hebu tusimwogope, bali hebu tumwamini.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

¹⁰⁵ Ee Bwana, uliyemfufua Yesu tena katika wafu, na umemwasilisha kwa Kanisa kujitangaza Mwenyewe kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, tuna furaha sana kwamba, kote ulimwenguni, kwamba tumeona makafiri wakija mkutanoni wakiwa na sanamu mkononi mwao, mchawi pamoja na uchawi wake wote, akijaribu kuurusha, na kumwona amesimama amepooza, amekufa ganzi kwa Roho Mtakatifu, kumwona ka—kafiri mwabudu wa kienyeji akivunja sanamu yake ardhini, akisema, “Mungu huyo na awe Mungu wangu,” Mungu mwenye nguvu, Wewe ni Yehova, Mungu wa nguvu, Mungu wa miujiza.

¹⁰⁶ Katika nchi ya uenyeji wetu, tuna furaha sana, Bwana, kuona hata wasomi na walimu wakiona njaa na kiu. Loo, Wewe ulisema, “Heri wenye njaa na kiu, maana watashibishwa.” Na kujua, siku hizi, ya kwamba watu mashuhuri wanaona Nuru ikitokea.

¹⁰⁷ Ee Mungu, tuna furaha, leo, kuwaona Israeli wakija katika nchi ya uenyeji wao, taifa, ile Nyota ya kale ya Daudi yenye ncha sita ikipepea kule, hao Wayahudi wakirudi, wakisema kamwe hawarudi wapate kufa katika nchi ya uenyeji wao, bali wamekuja kumwona Masihi. Mungu, tunajua basi kwamba siku zetu zimehesabiwa. Tunaangalia, kama tu vile Nuhu alivyomwangalia Henoko na kujua mara baada ya Henoko kuja hukumu itaipiga dunia, tunapona lile sanduku la Myahudi likitayarishwa tena, tunajua ya kwamba kule kuhamishwa kumekaribia. Tunangojea, Baba.

¹⁰⁸ Nasi tunaomba, usiku wa leo, katika kundi hili dogo ambalo Wewe umetupa, waliosimama pale mpaka viungo vyao vingi vinauma, ninaomba ya kwamba utawapa thawabu, Bwana, usiku wa leo, uwabariki. Hao wanawake na wanaume ambao ni wagonjwa na wana watoto wao wadogo hapa, jalia watulie tu sasa hivi, na kujua ya kwamba—ya kwamba silaha zote za Mungu ni za kimbinguni, hakuna kitu cha kawaida, zote ni za kimbinguni. Kwa hiyo kuwa Mkristo lazima tuamini mambo ya kimbinguni, kwa sababu, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana.” Nayo silaha ya Mungu ni upendo, furaha, imani, amani, uvumilivu, wema, upole, unyenyekevu, subira, Roho Mtakatifu. Hizo zote hazionekani, bali ni halisi, hazifi, zinaishi milele.

¹⁰⁹ Tunajua ya kwamba tunawapenda wapendwa wetu, hata tungeweza kuwaweka mikononi mwetu, watoto wetu wadogo, na

kuwakumbatia, na kuwavuta, na hata hivyo, hatuwezi kujisikia kuridhika, tunataka kuvuta nafsi zetu ziingie ndani ya nafsi zao.

¹¹⁰ Tunaiangalia dunia ikishuka leo, na kuona nyasi zikifa, miti ikifa, nami nikawazia, “Naam, Bwana, nami nafa, na ulimwengu mzima unakufa, hakika, kuna Ulimwengu mmoja mahali fulani unaoishi.” Hebu na tuweke dira yetu na nanga yetu usiku wa leo, tuabiri tunapoondoka kwenye bandari ya dunia hii, kuruka kwa imani hata Kwake Yeye aliyetoa ahadi.

¹¹¹ Sasa, Baba, imeombwa ya kwamba—ya kwamba ningefanyiza mstari wa maombi usiku wa leo, kusudi watu wapate kukuona Wewe ukija na kufanya kazi ambazo ndio kwanza tuzungumzie. Ulisema, “Mtu akiniamini Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Na, hivi wanafunzi walijua ya kwamba huyo hapo alikuwa Masihi, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara Yake.

¹¹² Nawe ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Lutu.” Nasi tunatambua ya kwamba wakati siku za Ibrahimu, kwamba kulikuwa na Billy Graham wa kisasa aliyeshuka kwenda Sodoma akahubiri Injili, na kumtoa Lutu, kanisa la kawaida, bali Kanisa hilo la kiroho, Ibrahimu, Sara, kulikuwako na Mtu aliyekaa pamoja nao aliyeonyesha ishara ya mambo ya kimbinguni.

¹¹³ Wakati alipokuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, Yeye alisema, “Yu wapi Sara, mkeo?” Alijua je kwamba alikuwa na mke? Alisema alikuwa mgeni.

Kasema, “Hemani nyuma yako.”

¹¹⁴ Naye akamwambia angemtembelea, katika muhula wake, naye Sara, ndani ya hema akacheka, moyoni mwake, ndipo Malaika akasema, “Kwa nini akacheka?” Hiyo ilikuwa ni ishara, muda kidogo tu kabla ulimwengu haujateketezwa.

¹¹⁵ Ulisema kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika siku hii. Mungu, ungali una Malaika, nasi tunatambua ya kwamba Malaika alidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, kwa kuwa muda si muda Yeye alitoweka mbele ya Ibrahimu, naye Ibrahimu akamwita *Elohimu*, Mungu.

¹¹⁶ Sasa, Bwana, njoo kwenye miili yetu na ututakase usiku wa leo, na uonyeshe ishara zile zile ulizoonyesha huko Sodoma, ili kwamba kukiwako na asiyeamini aliyesimama, ama aliyeketi mahali fulani, ili waweze kuona kwamba tuko kwenye wakati wa Moto, kwa kuwa ulikuwa ni Moto katika siku za Lutu, wakati Malaika huyu alipojitambulisha Mwenyewe. Mtume usiku wa leo, Baba, tunajitolea kwa Roho Wako Mtakatifu, jalia afanye mambo ambayo Yesu alifanya, kama alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake.

¹¹⁷ Ndipo basi, alipofanya hivyo, mbele ya Kleopa na mwanafunzi mwingine, wakati alipokuwa nao wamejifungia

chumbani, walipokuwa wakienda zao nyumbani, walisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo Yeye alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa sababu alifanya jambo kama alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, walijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Bwana aliyefufuka.

¹¹⁸ Sasa, Baba, fanya mambo yale yale miongoni mwetu usiku wa leo ambayo hao wanafunzi walikuwa wakizungumzia katika ile meli ndogo, tuliyozungumzia usiku wa leo. Wengi watahuka kwenda mtaani wakisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina. 

60-1124 Ni Mimi
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org